kumekucha @kumekucha @kumekucha

mwanzo mpya

# KUMEKUCHA

Tovuti: www.kumekucha.co.tz | ISSN 4562-9710 Toleo Na.Toleo 0009 ALHAMISI JANUARI 30, 2025 / Bei Tsh 1,000 Ksh 100



# Stephen Wasira 'amchanachana' Lissu

>> Asema Dk. Samia alimfutia kesi Mahakamani, Amtaka akumbuke fadhila za Dk.Samia Msukuma aisagia kunguni Chadema

# Mbowe aipotezea CHADEMA



>> Aingia mitini kumkabidhi ofisi Lissu,Mnyika afunguka

## Ifahamu nguvu ya kisayansi 'inayoikinga' Pwani ya Afrika Mashariki na Vimbunga

10

*Rais wangu, nilifuatilia na kukumbana na ubabaishaji mkubwa katika ile mikopo ya asilimia 10 ya*

## Barua ya wazi kwa Rais wangu Dkt. Samia



# Donal Trump hapoi

# Stephen wasira 'amchanachana' lissu

Na Mwandishi Wetu

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM - Bara, Stephen Wasira,amemchana Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA)Tundu Lissu,akisema ni mtu asiyekuwa na shukrani licha fadhila za kufutiwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kupitia falsafa ya 4R.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kata ya Kakubilo wilayani Geita Mkoani Geita,Wasira,alisema,Lissu alikuwa na kesi sita mahakamani ambazo aliwasilisha maombi kwa Dk.Samia afutiwe yeye na wanachama wengine wa chama hicho na Dk.Samia akafanya hivyo kupitia mamlaka aliyonayo kikatiba lakini jambo la kushangaza ni kumuona Lissu anabeza siasa za maridhiano ambazo ndizo zilizomuokoa.

Alisema, CHADEMA na viongozi wake walipewa nafasi ya kukaa na kujadili mambo mbalimbali kuhusu mustakbali wa maridhiano.

"Chadema waliwasilisha hoja 11,kwanza walitaka wanachama wao waliokimbia nje ya nchi warudi nchini akiwemo Tundu Lissu ambaye alirejea nchini,jambo lingine ni kuhusu wanachama wa chama hicho ambao walikuwa na kesi mbalimbali akiwemo Lissu na wengine walikuwa wamefungwa jela ambapo walitoka kwa msamaha wa Rais.

"Pia, walitaka kuruhusiwa mikutano ikaruhusiwa na wakaja mpaka huku lakini hawakuwa na jambo."Jambo ambalo lilishindikana ni kuwafukuza wabunge wa viti maalumu ambao jambo lao lilikua lipo mahakamani," alisema.

Wasira alisema,jambo lingine ni kuhusu katiba mpya ambapo walitaka iandike kwa siri "sisi tukasema hatuwezi kufanya siri jambo la wananchi na hapo ndipo tulipoishia wakaamua kutoka tena kwa hiyari sasa waliingia kwa hiyari wametoka kwa hiyari."

Aidha, Makamu Mwenyekiti wa CCM alitoa angalizo kwa viongozi wa CHADEMA) wanaotaka kutumia hoja ya umri wake kama mtaji wa kisiasa na kuwataka wajipange vyema.

Alisema CCM imejipanga kwa kila namna kuwaletea maendeleo wananchi na haitayumbishwa na hoja dhaifu."Wako watu wanahoji na kusema tumekaa miaka mingi madarakani, hii ni hoja dhaifu kwani tulipokuwa tunapigannia uhuru tuliingia mkataba wa kukaa madarakani kwa muda gani.

"Nataka tuwaambie kuwa bado tutakaa sana madarakani, hatuna mpango wa kutoka kwa kuwa tunaongoza kwa ridhaa ya wananchi," alisema.

**HOJA YA UMRI**

Alisema viongozi wa CHADEMA akiwemo mwenyekiti wake Tundu Lissu na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho John Heche kwamba Wasira ni mzee, hiyo ni hoja dhaifu kwa kuwa ana uwezo mkubwa wa kiutendaji hususan katika siasa.

"Ukiona mtu anasema sema ujue sindano imemfikia,hatuwezi kubishana na kibaka, "Tunakwenda na Falsafa ya 4R ambazo muasisi wake ni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. Njooni tuzungumze hatuwezi kubishana," alisema.

Alisema licha umri wake mkubwa lakini na uwezo na kwamba umri mkubwa sio kigezo cha kushindwa kuwajibika.

"Wakaulize Wamarekani hivi karibuni walifanya uchaguzi na wakaamua kumchagua Trump ambaye ana umri kama wangu wakamuacha Camara ambaye ana miaka 60," alisema.

Alisema 'wao wanadhani mawazo ni umri "mimi nina umri mkubwa lakini nina mawazo ya miaka 55 na gari ni injini siyo bodi, kama anataka ushahidi aende Muhimbili au India.

Katika Mkutano huo Mbunge wa Geita aliwaambia maelfu ya watu waliohudhuria kuwa katika uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu CCM haitakuwa na kazi kubwa ya kumnadi mgombea wake Dk.Samia Suluhu Hassan kwani amefanya maendeleo makubwa kupitia miradi ya kimkakati ambayo inatosha kumpa ushindi wa kishindo.

Alisema,CCM haiwezi kutishwa na wanasiasa aina ya Lissu na Heche ambao hawana kitu cha kukinadi chama chao mbele ya wananchi kutokana na mendeleo makubwa ya kiuchumi yaliyofanywa na Dk.Samia.

## RAIS SAMIA AFANYA UTEUZI

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa viongozi mbalimbali. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka, walioteuliwa ni kama ifuatavyo:

Jaji Mstaafu Beatrice Rhoda Mutungi ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Rufani za Kodi (TRAT). Jaji Mstaafu Mutungi anachukua nafasi ya Jaji Mstaafu Gad John Mjemmas ambaye amemaliza muda wake.

Dkt. Diwani Bakari Msemo ameteuliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI). Dkt. Msemo ni Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Saratani, anachukua nafasi ya Dkt. Julius David Mwaiselage ambaye atapangiwa majukumu mengine.

CPA David Carol Nchimbi ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya NMB Plc. CPA. Nchimbi anachukua nafasi ya Dkt. Edwin Mhede ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.



## TANAPA wapigwa msasa

Na. Edmund Salaho – Ziwa Manyara

VIONGPZI wa Idara mbalimbali ndani ya Makao Makuu ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)wameanza mafunzo maalum ya siku tatu katika ukumbi wa mikutano wa Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara kuhusu Uhamasishaji wa Usimamizi wa Vihatarishi vinavyoweza kuathiri utendaji kazi wa TANAPA (Risk Management).

Akifungua mafunzo hayo Naibu Kamishna wa Uhifadhi na Maendeleo ya Biashara, Massana Mwishawa aliwataka viongozi hao kutoka Makao Makuu ya Shirika kutambua jukumu kubwa la kusimamia na kupunguza vihatarishi ili kutekeleza majukumu ya Shirika kwa ufanisi mkubwa.

" Lengo la mafunzo haya ni kuwapatia zana za vitendo, maarifa, na mikakati ambayo itatumika kuboresha usimamizi wa vihatarishi katika taasisi nzima,TANAPA tunatekeleza muongozo wa usimamizi wa viatarishi (Enterprise Risk Management Framework and Policy 2024/2025 - 2028/2029)."

Aidha, Kamishna Mwishawa aliongeza kuwa vihatarishi ni jambo lisiloweza kuepukika. Hivyo, ni muhimu kila mmoja hasa wale walioko katika nafasi za uongozi kuwa na uelewa thabiti wa jinsi ya kushughulikia changamoto hizi kwa ufanisi .

## Mufindi na kampeni ya mti wa Mama

Na Man Kay Anton

"Kitakachowagusa wananchi wa chini ni huduma bora tutakazotoa, tutoe huduma sawa kwa wananchi bila kuwa na matabaka kwa kufanya hivyo miundombinu iliyoboreshwa katika Hospitali hii ya Mji Mafinga iliyojengwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu itafanya wananchi kupata huduma bora na kuisemea Serikali vizuri.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Mufindi,Dkt. Linda Salekwa,alipokuwa akizindua zoezi la Upandaji wa Miti katika Halmashauri ya Mji Mafinga ( MTI WA MAMA) zoezi lililofanyika Katika Hospitali ya Mji Mafinga kwa kushirikisha wadau wa PRESHDAS Company Limited ambao wametoa jumla ya miche 570.

Alisema Majengo yaliyojengwa katika Hospitali ya Mji Mafinga yataenda kuwa na maana kama mazingira ya Hospitali na huduma yatafanana na majengo.

" Tuhakikishe mazingira yanayoizunguka Hospitali ya Mji Mafinga yanaendelea kuboreshwa kwa kupanda ukoka, maua na kuweka maeneo ya kupumzika kwa wagonjwa

Aidha Mkuu wa Wilaya alimpongeza Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Mafinga Regnant Kivinge na Mkurugenzi Mji,Fidelica Myovella kwa kuamua kuchagua Hospitali ya Mji Kupandwa Miti na kupongeza kwa kujenga jengo la Kuifadhia Maiti na jengo la wodi ya daraja la kwanza( VIP) kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

## Mbowe 'ampotezea' tundu Lissu

NA HUSNA NASSORO

**KATIKA hali inayoashiria kwamba bado mambo hayako sawa ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA),Mwenyekiti wa zamani wa Chama hicho Freeman Mbowe ameingia mitini baada ya jana kushindwa kutokea Makao Makuu ya Chama hicho Mikocheni jijini Dar es Salaam katika hafla ya kumkabidhi ofisi Mwenyekiti mpya wa Chama hicho Tundu Antiphas Lissu.**

Itakumbukwa Mbowe na Lissu walikuwa kwenye mnyukano mkali wa uchaguzi Mkuu wa Chama uliofanyika Januari 21 mwaka huu ambao uliwaingiza katika kampeni za kurushiana vijembe,kashfa hatua ambayo ilikiingiza chama hicho kwenye mpasuko.

Kitendo cha Mbowe kushindwa kutokea katika makabidhiano hayo kinaelezwa na wachambuzi wa masuala ya siasa kuwa ni ishara ya maumivu aliyonayo moyoni baada ya kuangushwa na Lissu lakini makovu ya amkombora aliyokuwa akirushiwa n mpinzani wake huyo wakati wa kampeni za kutafuta Mwenyekiti wa chama hicho.

Itakumbukwa katika hotuba yake kufunga Mkutano wa Uchaguzi Mbowe licha kukubali matokeo lakino alisema, uchaguzi huo umeacha majera makubwa kwa wanachama wa chama hicho na hivyo kuwaomba viongozi walioingia madarakani kuunda Kamati ya maridhiano ili kuleta umoja ndani ya CHADEMA.

Akijibu hoja ya kwanini Mbowe hakutokea katika makabidhiano hayo, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika,alisema,Mwenyekiti huyo habanwi na kanuni yoyote inayomtaka kufika kwani ofisi zote ziko chini yake yeye.

"Ofisi na mafaili ya Chama yako chini ya Katibu Mkuu na hivyo zoezi la kukaribishwa na kukabidhiwa ofisi kwa Mwenyekiti wetu Lissu liko chini yangu,hivyo Mbowe hakuwa na ulazima wa kuwepo na hakuna kanuni yoyote ya chama iliyovunjwa,"alisema Mnyika.

Katika hafla hiyo Lissu aliwasili Makao Makuu ya Chama hicho akiwa ameambatana na Makamu Mwenyekiti,Bara, John Heche na Naibu Katibu Mkuu Bara Amani Golugwa kwa ajili ya kuanza rasmi majukumu yao mapya.

Lissu na ujumbe wake walipokelewa na Mnyika pamoja na Watendaji wengine wa Makao Makuu ambapo alizungumza na Waandishi wa Habari na kusema, kuelekea uchaguzi Mkuu CHADEMA haijasema itasusia uchaguzi kupitia kampeni yao 'No Reform No Election'.

."Kuna uchaguzi mkuu mwezi Oktoba mwaka huu na kuna no reform no election (hakuna mabadiliko, hakuna uchaguzi) hayo mambo mawili hayaendi pamoja kwa maoni yangu, sisi hatujazungumza kususia uchaguzi tunasema hakuna mabadiliko hakuna uchaguzi, lazima tuzungumze hayo mambo mawili tuone tunawezaje kwenda nayo mbele, aidha kwa pamoja au tuamue lipi ni muhimu zaidi, sasa hiyo sitaki kuzungumzia hapa tunaenda kujifungia tujadili"

"Tutakaa kwenye vikao tutatoka na msimamo wa Chama, sasa inabidi tuzungumze lugha pekee anayoweza kuielewa Samia Suluhu Hassan na tutaizungumza, nani anataka uchaguzi kama wa mwaka jana, wa 2020 au 2019, anyooshe mkono hapa, no reform no election, na tutazungumza lugha ambayo Samia Suluhu Hassan ataielewa"

"Na tutazungumza hadharani mchana kweupe, hatuna ajenda ya siri, tutaongea na Ndugu zetu duniani tutawaambia watuunge mkono hadharani, tutajifungia, tutakuja na mpango, katika siku ya kwanza ofisini nafikiri tumeanza vizuri, hao wanaosema hawa Wabangaizaji wataendesha Chama tumewathibitishia tunaweza" alisema Lissu.

## CHADEMA yaipa somo Serikali

HUSNA NASORRO

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetoa mapendekezo matatu kwa serikali kufuatia uamuzi wa Rais wa Marekani,Donald Trump kusitisha misaada kwa sekta ya afya.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana Mwenyekiti wa Kamati ya Afya na Maendeleo ya Jamii ya Bunge la Wananchi CHADEMA, Ashura Masoud, lazima hatua zichukuliwe kukabili mabadiliko hayo.

Chama hicho kimependekeza serikali kuandaa mkakati wa dharura wa kisera na kibajeti wa kuhakikisha inakuwa na fedha za kutosha kwenye Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI na Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI kwa kubana matumizi na kutenga vyanzo maalum na vya lazima katika bajeti ya taifa,ili kupunguza makali ya uhaba wa fedha za ARVs na UKIMWI.

Pia Bunge linaloendelea sasa kujadili ajenda ya dharura,serikali iwasilishe taarifa ya tathimini na mkakati wa kina wa namna ya kukabiliana na upungufu wa fedha katika sekta ya afya na nyingine za maendeleo,kisha litokea na azimio.

## Donald Trump hana kupoa

RAIS Donald Trump ametoa agizo la kusitisha utoaji wa mikopo na ruzuku zote za Serikali kuu ya Marekani hatua ambayo inatarajiwa kuathiri Sekta muhimu kama Elimu, Afya, Makazi na misaada ya maafa Nchini humo.

Hatua hii imeibua wasiwasi miongoni mwa Viongozi wa Serikali za mitaa na Mashirika yasiyo ya kiserikali wakihofia athari za kiuchumi na kijamii zitakazotokana na kusitishwa kwa fedha hizo pia Wakosoaji wanasema kuwa hatua hii inaweza kusababisha kusimama kwa huduma muhimu zinazotegemea ruzuku na mikopo ya Serikali kuu.

Kwa upande wake Ikulu imetetea uamuzi huo kupitia Ofisi ya Usimamizi na Bajeti ikisema kuwa hatua hiyo inalenga kufanya mapitio ya kina ya matumizi ya fedha za Serikali na kuhakikisha kuwa zinaendana na vipaumbele vya utawala wa Rais Trump.

Hata hivyo Mawakili Wakuu wa Serikali kutoka majimbo kadhaa wametangaza mpango wa kufungua kesi kupinga hatua hiyo wakidai kuwa itaathiri vibaya maisha ya Wananchi wa kawaida hasa wale wanaotegemea huduma za kijamii zinazofadhiliwa na Serikali kuu.

# Jokate Urban Mwegelo

## Katibu wa UVCCM anayezidi kupasua anga kisiasa

**OKATE Urban Mwegelo ni mwanasiasa mahiri na thabiti katika kizazi cha pili cha uongozi baada ya kizazi cha marehemu baba wa Taifa, Mwalimu Julias Kambarage Nyerere kuhitimisha kazi ngumu ya kulijenga taifa lenye Umoja na mshikamano wa viwango vya juu.**




Huyu ndiye Katibu Mkuu mpya wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi(UVCCM)ambaye Jumatano wiki hii Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM ilimteua kushika wadhifa huo.

Mwegelo mwenye miaka 37 ni miongoni watanzania na wanasiasa wachache wenye uwezo mkubwa wa akili zenye upeo wa juu sana waliohitimu chuo bora cha kizalendo Tanzania chuo kikuu cha Dar es Salaam na kupata ufaulu wa juu fani sayansi ya siasa na falsafa ( yaani Political Science and Philosophy).

Ni msomi aliyepikwa kuwa mwanasiasa mahiri,mbunifu na mwanamikakati asiyesubiri matokeo anayatafuta matokeo na kuthibitisha yeye mwenyewe.Nyota yake ya kisiasa inazidi kung'ara baada kupewa kuongoza kundi kubwa la vijana wa Tanzania wanaotazamiwa sana na CCM kuirudisha ikulu 2025.

Ni mwanasiasa mahiri na thabiti katika kizazi cha pili cha uongozi baada ya kizazi cha Nyerere na Bibi titi kuhitimisha kazi ngumu ya kulijenga taifa lenye Umoja na mshikamano wa viwango vya juu.

Kwa uchache Jokate kabla jina lake kutajwa medani za kisiasa ametoa mchango mkubwa kugusa familia maskini kote nchini hasa vijana vijijini na mijini.Ushawishi wake hapa nchini siyo wa kutilia mashaka ni miongoni mwa vijana maarufu sana na mwenye uwezo wa kujenga hoja kwa maslahi mapana ya taifa.

Mafanikio makubwa ya Jokate yalimfanya kuaminiwa na serikali ya Tanzania kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe ambako alifanya mapinduzi makubwa ya kimaendeleo pamoja na kufanya mageuzi makubwa ya elimu wilaya ya kisarawe.

Alipohamishiwa Wilaya ya Temeke jiji la Dar es Salaam akishirikiana na miongoni mwa wakurugenzi bora kwa uchapakazi Tanzania ndugu Elihuruma Mabelya walipata mafanikio makubwa kwenye makusanyo ya mapato kuongoza Tanzania na kusimamia mapinduzi ya matumizi bora ya rasilimali za serikali kwa uzalendo mkubwa wilaya ya Temeke.

Alipokwenda Korogwe kama Mkuu wa Wilaya akaibadili Korogwe kutoka vijiji vya kimaskini na kuifanya kuwa na hadhi ya Mji unaokimbia kimaendeleo kwa kasi.CCM kwa kutambua uchapakazi wake wakamteua kuwa Katibu wa Umoja wa Wanawake wa CCM Tanzania(UWT) ambako amefanya mapinduzi makubwa kuunganisha wanawake wote wa chama hicho huku mwenye kukemea uzembe na kutaka uwajibikaji kila ofisi UWT.

Tayari vikao vya ngazi ya juu CCM vimempa imani ya kuhudumia kundi kubwa la vijana wanaotazamwa sana 2025 kushiriki uchaguzi mkuu. Kifupi uchaguzi wa 2025 vijana ndiyo watakaoamua juu ya taifa lao pengine kuliko hata akina mama.. tulizoea kuwa ndiyo wapiga kura wakubwa. Hesabu za CCM kwa Jokate Urban Mwegelo ni bora sana katika siasa za sasa Tanzania.

Imeandikwa na Chigaitan Mapinduzi Vijijini ambaye ni mwandishi wa kitabu Mapinduzi vijijini,mchambuzi wa masuala ya kisiasa na diplomasia Tanzania( na Afrika).

**0757900020.**



## Madaktari, Maprofesa, Mainjinia kujaa Bungeni!

# Na Onyo la Mwalimu Nyerere juu ya Elimu ya Kikoloni

A HUSNA NASORRO

**ILIKUWA ni nadra sana pale Baba wa Taifa Mwalimu Julis Nyerere alipohitimisha hotuba yake inayohusu elimu bila kutoa onyo juu ya urithi hatari wa Elimu ya Kikoloni kwa kizazi cha Watanzania.**



Alionya kwa maneno makali katika na kusisitiza kwamba, watoto wa Kitanzania wakiipenda Elimu ile kisha wakaamua kuacha msingi yao na kuifuata, basi itazalisha taifa lenye watu wavivu wasiopenda kufanya kazi hasa za mikono.

Nukuu yake moja juu ya Elimu hatari ya Kiloni alisema, Nanukuu "Ile Elimu tuyorithi kwa Wakoloni siyo nzuri, ilitutenga Elimu na kazi vikawa vitu mbalimbali.

Mwanafunzi alikuwa mahiri sana kusoma Kiingereza, Mwandiko wake safi sana, Historia kwake ni mchezo, ila kufua nguo zake tu hawezi na kufagia nyumba pia hawezi, kulima hoi na kazi yoyote ya mikono kwake ni sumu" mwisho wa kunukuu.

Msisitizo enzi ya utawala wake wa Awamu ya Kwanza akiiongoza Tanganyika na hatimaye Tanzania Huru, Mwalimu alisisitiza Elimu ya Kujitegemea ndiyo itakayomwezesha kijana kujitegemea pindi atakapomaliza masomo yake.

Waliosoma nyuma ya miaka ya 1990 watakumbuka vizuri masomo kama EK (Elimu ya Kujitegemea) au hata kabla ya hapo lilijulikana kama Somo la Maarifa ya Nyumbani, pia Siasa ni Kilimo.

Katika uboreshwaji wa Elimu ile ya Kujitegemea shule mbalimbali za Msingi na Sekondari enzi hizo zilikuwa na madarasa yanayofundisha kazi za mikono kwa vitendo.

Wanafunzi walitumia nafasi hiyo kujifunza ufundi Seremala, Uashi, Kilimo Ufungaji, Upishi na mengine kadhalika, ikiwa ndiyo Elimu inayoweza kumlea mtoto wa Kitanzania ili atakaomaliza masomo yake apate maarifa ya kufanya kazi kazi alizojifunza shuleni.

Masomo haya ndiyo Chimbuko la Watanzania wengi wa enzi hizo kujikita katika masuala ya ufundi, hili kwa kiasi kikubwa lilipunguza kilio cha kuwepo vijana wengi wanaosota vijiweni kwa kisingizio cha kutokuwa na kazi.

Walipyatumia masomo yale vizuri waliweza kujiaridi kisha nao wakaajiri wenzao na kuzidi kuzalisha mafundi walioijenga nchi kwa kiasi kikubwa.

Hata wakulima enzi zile walikuwa na utaratibu wa kutenga siku moja au mbili kati ya wiki na kwenda kulima mashamba ya Ushirika ili kuweka akiba ya pamoja ambayo ingesaidia kusogeza maendeleo ya pamoja katika eneo lao.

Kwa kiasi kikubwa Elimu na Maarifa yale yalikuwa yakiyeyuka polepole na hatimaye kubaki katika historia, endapo mtu atahitaji kusoma anaweza kuyakuta maandiko yaliyojaa katika maktaba zetu.

Hakuna tena masomo yale ya vitendo hata yakiwepo siyo ya aina ile bali yameingia katika misingi ya kibiashara, mathalam mwanafunzi atahitajika kwenda kusoma Chuo cha Ufundi kwa kulipiwa ada ili ajiandae kupata elimu ya ufundi.

Mazoea haya ndiyo yaliyojenga ari hasi kwa vijana wa Kitanzania wakajikuta wanasomea taaluma walizozikuta wakiwa watu wazima, hawakuanzia shule zaawali kuelimishwa juu ya faida yake.

Hawakujulishwa manufaa ya kusomea ufundi na baadaye kuwa Injinia na nini ataweza kufanya kama itabidi kujitegemea!

Hatimaye leo tunazidi kuzalisha Madaktari, Mainjinia na wasomi wanaokesha wakisoma 'Vitabu vya Uinjinia' au 'Udaktari', lakini ndoto zao zikiwa ni kufanya kazi za Siasa na hasa Bungeni, ambako kiuhalisia hakuhitaji wasomi wa kupindukia na wengi kiasi hiki ilivyo kwa sasa.

Bungeni hakuna dharura ya kuwafanya Madaktari waachane na tiba Mahospitalini ili waende wakatetee wananchi wanaokumbwa na changamoto za kilimo au miundombinu.

Hazikutangazwa nafasi zawahasibu kule wakaachana na kazi zao na mahesabu na kupambana kufa na kupona ili waingie Bungeni.

Hakukuwa na uhaba wa Wahandisi walioombwa kuacha kubuni majengo na kujenga barabara zetu, badala yake waende wakaondoe shilingi katika bajeti wanazopingana nazo kule Bungeni.

Haya ndiyo mabadiliko tunayoyashuhudia hasa wale wenzangu na mie tuliyebahatika kuonja awamu zote za uongozi wa taifa hili.

# MILIMA YA UDZUNGWA NA MAAJABU YAKE



NA VICTOR MAKINDA

**UTALII ni kitendo cha mtu au kundi la watu kutoka eneo moja kwenda eneo jingine kwa lengo la kujionea kumbukumbu za kihistoria au vivutio vya aina nyingine kama vile wanyama, misitu, mito mikubwa, bahari majengo au inaweza kuwa kitu kingine chochote kama vile maeneo ilipopiganwa vita, maeneo waliyozaliwa watu maarufu ama viongozi wa dini.**

Utalii una umuhimu mkubwa katika ustawi wa maisha ya biniadamu. Pamoja na kuwa ni kiburudisho cha akili lakini pia utalii unaongeza ufahamu kuhusu mazingira na vitu mbali mbali Mwenyezi Mungu alivyovumba ambavyo vinavyoipamba Dunia yetu nzuri.

Hifadhi ya Milima ya Udzungwa, inayopatikana katika mikoa Morogoro na Iringa ni moja ya eneo lenye mvuto wa kipekee wa kitalii. Hifadhi hii ya Milima ya Udzungwa ni nyumbani kwa aina nyingi za wanyama, mimea,aina tofauti toauti za ndege na viumbe vingine ikiwa ni pamoja na maporomoo makubwa ya maji yanayojulikana kama maporomoko ya maji ya Sanje.

Utajiri wa Maliasili za hifadhi hii ni mkubwa. Ni eneo lililotuzwa vizuri na lenye uoto wa asili unaovutia, jambo ambalo linaipa akili ya mtembeleaji/mtalii wa hifadhi hii uwezo wa kujifunza na kujionea utajiri mkubwa wa maliasili ambazo Mungu ametujalia sisi Watanzania.

Kuelezea uzuri wa Hifadhi ya Milima ya Udzungwa kunahitaji kurasa nyingi zaidi. Kama nilivyokwisha kusema awali, Hifadhi ya Milima ya Udzungwa ina aina nyingi za mimea viumbe na wanyama.

Katika kundi la wanyama linalojulikana kwa lugha ya kimombo kama Big Five, ikiwa inawajumuisha, Simba, Tembo, Kifaru, Twiga na Chui, mnyama mmoja tu ambaye ni Kifaru ndiye hapatini hifadhini hapo.

**UPEKEE WA HIFADHI YA MILIMA YA UDZUNGWA**

Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa yenye vilele vingi kikiwemo kilele kirefu zaidi katika hifadhi ya milima hiyo, kilele cha Ruhomero chenye urefu wa mita 2576, ina aina 2500 za mimea huku ikiwa na maporomoko mengi ya maji yakiongozwa na maporomoko marefu zaidi kuliko yaliyopo Hifadhi zote za Taifa, maporoko ya maji ya Sanje yajulkanayo kama Sanje Water Fall.

aporomoko hayo yana urefu wa mita 1978. Maporomoko mengine ya maji katika Hifadhi hiyo ni Prince Bernard, Njokamoni. Ndani ya Hifadhi hii ya Milima ya Udzungwa kuna mapango makubwa yaliyobeba historia ya biashara ya utumwa na vita uliyopiganwa kati ya wahehe na Wajerumani.

Licha ya mapango hayo kubeba historia ya biashara ya utumwa ni mahali muhimu kwa ibada za jadi. Mapango maarufu yanayopatikana katika Hifadhi hiyo ni Mwanaburele, Mwanihana, Nyumba Nitu, Mdene.

Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa ina mengi mazuri yenye kuvutia ambapo orodha yake ni ndefu. Kuna aina nyingi za mijusi, akiwemo mjusi pekee anayepatikana katika hifadhi hii na hapatikani mahali pengine Duniani. Mjusi huyu maarufu anayejulikana kwa jina la Udzungwa Rizard ni miongoni mwa vivutio vikubwa vya watalii katika hifadhi hiyo.

Umaarufu wa hifadhi ya Udzungwa nin pamoja kuwa ni hifadhi yenye aina nyingi za ndege kuliko hifadhi yoyote barani Afrika huku ikiwa na aina 400 za ndege.

Kati ya aina hizo 400 zinazopatikana katika hifadhi hiyo, aina mbili za ndege zinapatikana katika hifadhi hiyo tu na huwezi kuwaona ndege hao mahali pengine duniani.

Moja ya aina ya ndege hao ambao anatajwa kuwa ndege mkongwe kabisa Duniani ni kwale wa mistari, ambapo watafiti wanamtaja kuwa aliishi miaka Milioni 40 iliyopita.Aina hiyo ya kwale ipo hatarini kutoweka ambapo juhudi kubwa zinapaswa kuelekezwa katika kumuhifadhi ndege huyo adimu na adhimu.

Pia kuna ndege anayejulikana kama Chozi Mbawa Nyekundu au Sunbed, ambaye naye huwezi kimuona mahali pengine duniani.Hakika Hifadhi ya Udzungwa ni kisima cha utalii na mvuto wa kimazingira huku ikiwa kuna aina nyingi za nyoka katika hifadhi hiyo.

Katika Hifadhi ya milima ya Udzungwa pamegunduliwa aina mpya ya nyoka ikiwemo Duniani, aliyevumbuliwa na kuonekana kwa mara ya kwanza katika hifadhi hiyo hivi karibuni.

Nyoka huyo anayepewa jina la Matildaís horned Viper alibainika mwaka 2009 na kuthibitishwa kuwa ni aina mpya ya nyoka Duniani mwaka 2011. Pia ndani ya hifadhi hii kunapatikana aina ya kinyonga wa kipekee anayejulikana kama Bearded Pigmy Chamillion ambaye ni mfupi na rangi yake hubadilika taratibu tofauti na aina nyinginze za vinyonga. Sambamba na hilo, kuna kuna aina 1200 za vipepeo kati ya aina hizo, aina tatu zinapatika katika Hifadhi ya Milima hii tu na huwezi kuipata mahali pengine Duniani.

**KUHUSU MAPOROMOKO YA SANJE.**

Maporomoko ya Sanje ndani ya milima ya udzungwa ni eneo lenye utajiri mkubwa na kivutio kisicho kifani. Maporomoko hayo ndiyo nembo ya hifadhi hiyo,

Ukiwa njiani kwenda kwenye maporomoko hayo unakutana na madhari nzuri ya misitu minene ya kitropiki yenye hali ya hewa nzuri yenye kuburudisha nafsi.

Katika maporomoko haya maarufu ya Sanje unaweza kuona aina kumi na moja za wanyama aina ya nyani wanaopatikana katika hifadhi ya Udzungwa, huku aina mbili tu za wanyama hao unaweza kuiona katika hifadhi hiyo tu na si mahali pengine Duniani.

Aina hizo ni mbega wanaojulikana kama Ngorago au Sanje Crested Mangabay, na Mbega mwekundu,anayejulikana kama Iringa red Collubus Monkay. Nyani aina ya Ngoraga amefanyiwa uzoeshaji wa kitabia na biniadamu (Habituation) ambapo mnyama huyo hamUogopi biniadamu na mtalii anaweza kumsogela kwa karibu kabisa na hata kucheza naye.

Katika maporomoko hayo maarufu ya Sanje, kuna bwawa kubwa la asili mahali maji yanapotua, ambapo mtalii anaweza kuogelea pasipo madhara yeyote.

Kileleni mwa maporomoko hayo, mtalii anapata fursa ya kutazama kwa upana mkubwa madhari ya bonde la Kilombero, hususani mashamba ya miwa ya Kilombero huku akiburudika na hali ya hewa nzuri sambamba na sauti za ndege na maji yanayoporoka.

Mandhari nzuri ya maporomoko hayo yanatoa fursa kwa mtalii kupiga picha katika uwanda mpana.Yapo maeneo mazuri na salama ya kuweka kambi na kufanya hafla na sherehe ndogo ndogo (picnic) sambamba na kujifunza masuala ya uhifadhi.

**FAIDA ZA KUTEMBELEA HIFADHI ZA MILIMA YA UDZUNGWA**

Hifadhi ya Milima ya Udzungwa ni mahali salama kwa afya ya mwili na akili kwa mtalii yeyote anayeitembelea. Hifadhi hii ni Hifadhi ya kutembea kwa miguu huku usalama ukiwa umeirishwa kwa asilimia mia moja kujikinga na wanyama wakali.

Mtalii katika Hifadhi hii ana nafasi ya kuona kila anachokitaka kwa ukaribu zaidi kwani hii ni hifadhi ambayo mtalii anatembea kwa miguu.

Usalama ni asilimia mia moja kwa kuwa mtalii haruhusiwi kupanda milima peke yake pasipo askari wa wanyama pori na muongozaji wa watalii.

Hifadhi hii ni mahali pazuri pa kuimarisha afya ya mwili kwani licha ya watu wengi wa mijini kuzoea usafiri wa vyombo vya moto, ndani ya hifadhi ya Udzungwa ni mahali sahihi pa kunyoosha viungo na misuli kwani mtalii atatembea kwa miguu kwa umbali atakaona unamfaa.


Hii ni fursa nzuri ya kufanya mazoezi ya kutanua misuli na viungo huku ukiimarisha afya ya mwili na akili kwa kujionea viumbe, mimea, wanyama na madhari nzuri inayoburudisha na kuipa unafuu akili kutokana na msongo wa mawazo.

Gharama za kuitembelea hifadhi hiyo ni ndogo sana na kila mtanzania hata mwenye pato la chini anaweza kuimudu huku wakati maeneo ya malazi na chakula yanapatikana kwa gharama rahisi pia.



## Nyuma ya Pazia

# Hatari ya Jangwa kata ya Weruweru



NA MWANDISHI WETU

**KATIKA Kata ya Weruweru, wilayani Hai, Kilimanjaro, suala la uharibifu wa mazingira limeendelea kuwa changamoto kubwa, huku viongozi wa kijiji wakituhumiwa kuhusika katika vitendo vinavyohatarisha mazingira na kusababisha mafuriko.**

Wananchi wamedai kuwa viongozi hao wanashirikiana na watu wanaokata miti ovyo, hasa katika kingo za mito, hali inayosababisha madhara ya kimazingira na kijamii.

Viongozi watatu wa kijiji cha Kikavu Chini wanatuhumiwa kushirikiana na wakataji miti kwa manufaa yao binafsi. Viongozi hawa ni Mwenyekiti wa Kitongoji cha Madukani, Lazaro Shauri Ndelelio, Mwenyekiti wa kijiji cha Kikavu Chini, Kombo Hassan Kombo, na Mtendaji wa Kata ya Weruweru, Jenfrida Mkanga.

Wananchi wamedai kuwa viongozi hawa wamekuwa wakikata miti kinyume cha sheria kwa kisingizio cha kwamba miti iliyozunguka kingo za mito iko ndani ya umbali wa mita 60 kutoka mtoni, hivyo ni mali ya serikali.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Madukani, Lazaro Shuri Ndelelio, ambaye anatuhumiwa kwa kushiriki katika ukataji miti, anakanusha tuhuma hizo akisema, "Mimi ni kiongozi, kwa akili zangu zilivyo timamu siwezi kuona mtu anakata miti hovyo nikamuacha. Sisi hatuwezi kufanya vitu vya kijinga; tukiona mtu anafanya hivyo lazima tumfikishe kwenye vyombo vya sheria.

Hata hivyo, wananchi wanadai kuwa Ndelelio na viongozi wenzake hawachukui hatua yoyote dhidi ya watu wanaovunja sheria.

Mwenyekiti wa kijiji cha Kikavu Chini, Kombo Hassan Kombo, anasema: "Mara nyingi wananchi wanapoona jambo la uharibifu lazima wasukume lawama kwa serikali, lakini wanapowaona waharibifu wanashindwa kutoa taarifa kwa viongozi. Mtu wa kwanza kuruhusu wahalifu wapite ni wananchi.

Kuhusu idadi ya guta zinazotoka kijijini, ambapo awali zilikuwa zikionekana kuondoka zaidi ya kumi kwa siku, Mwenyekiti Kombo anasema kwamba zilikuwa zinabeba magogo yaliyosombwa na mafuriko, na hivyo ilikuwa ni halali kwa watu hao kuvuna.

Hata hivyo, wananchi wanajiuliza ikiwa vibali hivi vinatolewa kwa njia halali, au kama kuna maslahi ya kifedha kati ya viongozi na wahusika katika ukataji miti.Mtendaji wa Kata ya Weruweru, Jenfrida Mkanga, ambaye pia anashutumiwa kwa kushirikiana na viongozi wengine katika kulinda wakataji miti, amekana tuhuma hizi. Siwezi kusema hapana au ndiyo, sio rahisi. Kama kuna mtu ana uthibitisho aseme. Anadai kuwa wanaokata miti wanakuja na vibali kutoka Maliasili, ambayo inawaruhusu kukata miti hiyo kwa matumizi ya biashara.

Hata hivyo, wananchi wanadai kuwa viongozi hao wanahusika katika kufanya maamuzi ya kimafia kuhusu uharibifu wa mazingira, na kwamba wanashindwa kuchukua hatua kwa sababu ya maslahi yao binafsi.

Mmoja wa wananchi wa kijiji cha Kikavu Chini ambaye hakutaka jina lake litajwe, anasema: "Viongozi hao wanahusika kwa sababu wamekuwa wakishuhudia miti hiyo ikivushwa na kupelekwa kijiji jirani cha Newland kwa shughuli za uchomaji matofali. Walikuwa na jukumu la kuzuia, lakini hawakufanya hivyo.

Mafuriko yanayotokea kila mwaka katika maeneo hayo yanaongeza uzito wa tuhuma dhidi ya viongozi. Mwaka 2023, wananchi kwa kushirikiana na wahisani walifanikiwa kupanda miti 1,000, lakini mafuriko ya mwaka 2024 yalisababisha miti hiyo kusombwa na kuacha miti 87 pekee.

Hali hii inadhihirisha jinsi uharibifu wa mazingira unavyosababisha madhara makubwa, ikiwa ni pamoja na kupotea kwa mimea, wanyama, na athari nyingine za kimazingira.

Viongozi wa kijiji wanadai kuwa miti inayokatwa ni mali ya serikali kwa sababu iko ndani ya umbali wa mita 60 kutoka mtoni.

Inadaiwa kuwa, wakati mwingine ukataji miti hufanyika usiku, na viongozi wakiwaona wanadai kuwa miti hiyo iko ndani ya mipaka ya mto na ni mali ya serikali. Hali hii inazua wasiwasi kwa wakulima wanaozunguka maeneo hayo, ambao wanahofia kuwa uharibifu huu utaathiri mashamba yao na maendeleo yao ya baadaye.

Wananchi wa kijiji cha Kikavu Chini wanadai kuwa hakuna udhibiti wa kutosha wa shughuli za ukataji miti katika maeneo ya kingo za mto, na wanakosa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira. Hali hii inachangiwa na ukosefu wa mikakati ya kuzuia uharibifu wa mazingira kutoka kwa viongozi na taasisi zinazohusika na usimamizi wa misitu na mabadiliko ya tabianchi.

Hali ya uharibifu wa mazingira katika maeneo ya kingo za mito inahitaji umakini zaidi. Hata ingawa baadhi ya viongozi wanadai kwamba wanafanya kila wawezalo kulinda mazingira, ukweli ni kwamba baadhi yao wanatuhumiwa kwa kutoshirikiana na wananchi kwa manufaa ya kitaifa. Elimu ya utunzaji mazingira ni muhimu ili wananchi na viongozi waweze kufanya maamuzi sahihi kuhusu uhifadhi wa rasilimali za asili.

Hitimisho

Makala hii inaonesha changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira katika Kata ya Weruweru, Hai, Kilimanjaro, na jinsi viongozi wanavyohusishwa na vitendo vya uharibifu wa misitu, hususan katika kingo za mto Kikavu.

Tuhuma dhidi ya viongozi wa kijiji na mtendaji wa katazinaonyesha kuna ulazima wa kuimarisha usimamizi wa mazingira na kuhakikisha kwamba viongozi wanawajibika kwa matendo yao. Hali hii inahitaji mabadiliko ya kisheria, kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira, na kuleta uwazi zaidi katika usimamizi wa rasilimali za asili.

# Barua ya wazi kwa Rais wangu Dkt. Sami

NA HASSAN DAUDI

NIANZE kwa kukupongeza Rais wangu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kubwa ni historia uliyoiandika kwa wino wa dhahabu, ambayo itaendelea kusomwa katika siku zote za uhai wa Taifa hili.

Ndiyo, vizazi vijavyo vingi vitaendelea kuisoma na kuienzi historia yako ya kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa urais katika nchi hii.

Kabla ya kuingia kwako madarakani, haikuwahi kutokea kwa mwanamke kuwa rais wa Tanganyika, Zanzibar wala Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ukiweka kando hilo, licha ya muda mfupi uliokaa madarakani, yapo ya kutolea mfano, ambayo kimsingi yameonesha dhamira ya wazi uliyonayo katika kuhakikisha Tanzania inapiga hatua kubwa ya maendeleo.Sidhani kama inatosha kugusia kwa undani miradi mingi inayoendelea kutekelezwa chini ya Serikali yako ya Awamu ya Sita.

Tunaweza kukubaliana kwamba inahitaji si tu muda wa kutosha, bali pia nafasi kubwa zaidi ya hii niliyoipata katika gazeti hili.Kwa ufupi, safari zako za nje ya nchi, licha ya kwamba wapo wanaoponda, zimekuwa na tija kubwa katika nyanja ya uchumi.

Kila la kheri Rais wangu Dkt. Samia na nikuahidi kwamba kalamu yangu itaendelea kuwa nyuma yako, ikiwa haina chembe ya hofu katika kueleza mazuri yanayofanyika chini ya Serikali unayoiongoza.

Hata hivyo, Rais wangu, labda kuna baadhi ya mambo watu wako wa karibu wanahofia kukwambia. Sijui ni hofu, unafiki au ndiyo sifa sahihi ya utiifu mkubwa walionao kwako.

Kile wanachohofia kukwambia ni kwamba bado malalamiko ya ugumu wa maisha ni makubwa mno huku mitaani.

Licha ya jitihada kubwa ulizofanya tangu ukalie kiti cha urais, bado manung'uniko ya 'walala hoi' ni makubwa kutokana kupanda kwa gharama za maisha.Kilio cha wengi ni kupanda kwa bei na wakati mwingine kuadimika kwa bidhaa muhimu, ikiwamo mafuta ya kula, sukari, mchele na unga.

Wakati hilo la gharama za maisha likiendelea kung'ata, bado upatikanaji wa nishati ya umeme umeendelea kuwa 'pasua kichwa' kwa wananchi wako huku mitaani.Rais wangu, kutokana na uzoefu wangu mdogo wa maisha ya watu wa kipato cha chini, hii imekuwa ikiwaathiri mno wajasiriamali wadogo.

Katika hilo, najaribu kuwatazama wajasiriamali ambao wamechukua mikopo na kuwekeza katika biashara za kipato cha chini, nikizigusa saluni, vibanda vya vinywaji baridi (juisi, soda, n.k.)

Najaribu kukushirikisha Rais wangu; ni kwa namna gani wajasiriamali hao watamudu kurejesha mikopo kwa staili hiyo ya kufanya biashara isiyo na uhakika? Je, ni nani anayewakingia kifua mbele ya taasisi za fedha zilizowapa mikopo?

Sambamba na hilo, bado hali ni mbaya kwenye sekta binafsi. Katika nchi yao, wapo vijana 'wanaohenyeshwa' na kulipwa ujira kiduchu na kufanya kazi bila mikataba inayoilinda 'kesho' yao.

Huenda hata ...saidizi wako ...afahamu ...a hayo ...mekuwa ...kifanyika si ...katika ...mpuni zinazomilikiwa na wawekezaji wa kigeni, bali pia hata zile zilizo chini ya wazawa.

Rais wangu, hilo ni kando kabisa na hali mbaya ya shule zetu za kata, ambazo kwa macho tu unaweza kubaini kuwa zililenga watu wa kipato wa chini.

Bado changamoto ni uhaba wa walimu, huku pia ikishangaza kuona hata zile zilizoko maeneo ya mijini, ikiwamo Dar es Salaam, zina idadi kubwa ya wanafunzi wanaokaa chini kutokana na uhaba wa madawati.

Licha ya ufinyu wa nafasi, kama nilivyoeleza awali, nisiache kukukumbusha Rais wangu juu ya utitiri wa wahitimu wa elimu ya juu wanaoendelea kurundikana mitaani kutokana na uhaba wa ajira.

Walau kwa changamoto hiyo tunaweza kukubaliana kuwa hata mataifa yaliyoendelea, mathalan Marekani na Uingereza, hajayaweza kuipatia ufumbuzi wa kudumu.

Lakini, hiyo haimaanishi kuwa Tanzania inapaswa kuacha mikakati yake ya kukabiliana na ukubwa wa tatizo hilo, ikiwamo kuimarisha na kulainisha mazingira ya kupata mikopo ya kujiajiri.

Rais wangu, nilifuatilia na kukumbana na ubabaishaji mkubwa katika ile mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya halimashauri kwa wanawake, vijana na walemavu. Kwa sehemu kubwa, utekelezaji wake ulitokana na misingi ya kujuana, ufisadi na ukiritimba.

Licha ya hayo yote, nitumie fursa hii kukutoa hofu Rais wangu. Kwa utafiti wangu mdogo, nikiwa pia ni sehemu ya jamii, nimebaini kuwa licha ya changamoto hizo, bado uhusiano wako na wananchi ni mzuri.

Bado wengi wanaamini katika utendaji wako, wakikubaliana kwamba hiki ni kipindi cha mpito tu. Wengi wanakiri kuwa uchumi wa nchi unaendelea 'kujitafuta' baada ya kuyumbishwa na janga la Uviko-19.

Ikizingatiwa kuwa hii ni awamu yako ya kwanza madarakani, walio wengi wanaamini bado unahitaji muda wa 'kuziba ufa'.

Wakimaanisha, wako tayari kukuunga mkono katika Uchaguzi wa mwaka huu ili ukamilishe awamu mbili za kuiongoza Tanzania.Kila la kheri Rais wangu, Dkt. Samia.

**10**

***Rais wangu, nilifuatilia na kukumbana na ubabaishaji mkubwa katika ile mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya halimashauri kwa wanawake, vijana na walemavu. Kwa sehemu kubwa, utekelezaji wake ulitokana na misingi ya kujuana, ufisadi na ukiritimba.***



# KWANINI MTOTO ANYONYESHWE NUSU SAA BAADA YA KUZALIWA?



NA ANGELA KIBWANA

**KWANINI mama anashauriwa kumnyonyesha mtoto wake nusu saa baada ya kujifungua?**

**Kuna umuhimu mkubwa wa mama kumnyonyesha mtoto dakika 30 za mwanzo kwa sababu mtoto anapogusa chuchu ya mama, mwili wa mama unapeleka ujumbe kwenye ubongo wa mama kwamba mwili ujiandae kwa jukumu la kujiandaa kutengeneza maziwa ya mtoto.**

Sababu nyingine ni kwamba mtoto anapozaliwa katika dakika 30 za mwanzo inadhihirisha kwamba tayari mtoto amejifunza mambo ambayo hakujifunza akiwa tumboni,kwa hiyo kunyonyeshwa ndani ya nusu saa tayari anaanza kufundishwa kwamba mazingira aliyoishi akiwa tumboni ni tofauti alioko sasa kwa hiyo anaanza kujitegemea.

Sambamba na hilo mama huyu anapaswa kumnyonyesha mtoto wake kwa kipindi cha miezi sita bila kumpa chakula chochote, labda anaweza kumpa dawa kwa kufuata maelekezo ya daktari kulingana na hali ya afya ya mtoto huyo.

Ikumbukwe kwamba baada ya mtoto kufikisha miezi sita, mama anaruhusiwa kumwanzishia mtoto wake vyakula vya nyongeza ili kumuongezea chakula cha nyongeza baada ya kumnyonyesha maziwa ya kutosha baada ya kujifungua ingawa wanawake wengi wanakosea wengi wao wanawapa watoto kwanza vyakula vya nyongeza na baadaye kumnyonyesha mtoto, kwa hiyo kwa utaraibu wa lishe mama akifanya hivyo atakuwa amekosea.

Je kwa nini tunaanzisha chakula cha nyongeza  katika umri huu wa mtoto?

Hii ni kwa sababu mtoto huyu mwili wake sasa umekuwa kiasi kwamba maziwa ya mama hayawezi kumtosheleza, mwili wake unakuwa na uhitaji wa ziada wa nishati lishe ambazo kwa kipindi cha miezi 6 nishati hizo hazipati kwenye maziwa ya mama kwa utimilifu, hivyo mama anashauriwa kuongeza vyakula vya  nyongeza kutoka kwenye makundi matano ya chakula.

“Mtoto aongezewe vyakula vya jamii ya nafaka ndizi na mizizi ambalo ni kundi la kwanza, kundi la pili ni vyakula vyenye jamii ya mikunde na nyama ingawa kundi hili linamgawanyo baada ya wataalam kwa sasa wameona kwamba uwiano ulioko kati ya protin inayotokana na mimea na protin inayotokana na nyama uwiano wake hauko sawa”

Kundi lingine ni vyakula jamii ya mboga mboga, ambalo linajumuisha jamii ya mboga zote za kijani,na mboga zenye rangi ya njano mfano karoti,kundi la matunda lenye vitamini na nyingi na madini hivyo mchanganyo huo unamsaidia mama kupata kiasi cha nishati lishe inayohitajika kwa makuzi ya mtoto.

Afisa Mwahija anasema kuna udumavu dhahiri unaoonekana hasa mtoto akikosa lishe mfano ukondefu na udumavu uliojificha ambao unasababishwa na kutokuwepo kwa matumizi ya mbogamboga na matunda, udumavu huo unakuwa mwili na kuonekana baadaye mfano mtoto aliyekosa madini ya calcium anaweza kupata matege.

Madhara mengine ya kukosa lishe ni kwamba ,mtoto aliyekosa Vitamin A kinga yake inaweza kushuka na husababisha mtoto kupata homa za mara kwa mara, ikiwa ni pamoja na uoni hafifu hivyo ni jukumu la wazazi kuhakikisha wanazingatia kanuni za lishe bora.

Kwa upande wake Innocent Rusomyo afisa program wa asasi isiyokuwa ya serikali ya child hold development organization kwa ushirikiano na sekretarieti ya mkoa wa Morogoro katika kuratibu utekelezaji wa program jumuishi ya taifa ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kupitia mradi wa mtoto kwanza, anasema jamii inapaswa kuweka msukumo kwenye lishe ili kufikia lengo la kuwa na kizazi chenye afya bora.

Kwa mujibu wa umoja wa mataifa Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo asilimia 43 ya watoto wapo kwenye hatari hatua ya kutofikia hatua timilifu  za ukuaji kutokana na viashiria kama vile utapiamlo, umaskini na kukosekana kwa uhakika wa chakula.



# KAMWE USIDHARAU NGUVU YA MWANAMKE



ismas LYASSA

Saikolojia na Utafiti

**KAMWE usidharau nguvu ya mwanamke. Kwa ujumla ni wazalishaji, watumiaji na wabunifu. Wao ni mawakala wa kiuchumi wenye rasilimali, na kuthibitisha kila siku kwamba wanaweza kufanikiwa, mara nyingi katika uso wa vikwazo vya kijinsia vinavyoendelea.**

"Siku bila mwanamke" inamaanisha wanawake wachache wanaofanya kazi ili kuendeleza tasnia ya uzalishaji na huduma; wanawake wachache wanaotunza watoto, wazee na sisi sote; wanawake wachache wanaotumia pesa kwenye bidhaa zinazoendesha uchumi wetu. Kwa ufupi, wakati wanawake hawafanyi kazi, uchumi na jamii pia hazifanyi kazi.

Fikiria yafuatayo

Kupungua kwa pengo kati ya ushiriki wa nguvu kazi ya wanawake na wanaume - au kuongezeka kwa ushiriki wa nguvu kazi ya wanawake - husababisha ukuaji wa haraka wa uchumi.

Wanawake hudhibiti 70-80% ya ununuzi wote wa watumiaji.

Wanawake hufanya kazi mara mbili hadi kumi zaidi ya kila siku bila malipo kwa kupika, kusafisha, na kutunza washiriki wa familia. Hii ndiyo sababu wanaume katika takriban kila nchi wana muda zaidi wa shughuli za burudani, wakati wanawake wana muda mchache wa kazi, ushiriki wa kisiasa, na starehe zao wenyewe.

Wanawake hufanya yote haya licha ya mishahara, sheria, na kanuni za kijinsia ambazo zinaendelea kuwauza kwa muda mfupi. Mbali na kazi isiyolipwa, hakuna nchi ambayo bado haijapata usawa wa kijinsia au malipo sawa kwa kazi rasmi sawa.

Asilimia tisini ya nchi bado zina angalau sheria moja inayozuia fursa za kiuchumi za wanawake. Fikra potofu za kijinsia mahali pa kazi zinamaanisha kuwa wanawake wanatarajiwa kusaidia zaidi, hadi ambapo wanaume wana uwezekano mkubwa wa kupendekezwa kwa kupandishwa vyeo na kuinuliwa kuliko wanawake wanaotoa msaada sawa. Ikiwa wanawake walifunga pochi zao, tasnia ya watumiaji inaweza kukwama.

Ni wakati muafaka wa kujumuisha uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kama sehemu ya msingi ya uchumi unaostawi.

Uwekezaji katika uwezeshaji wa wanawake kiuchumi pia ni uwekezaji katika jamii nzima. Wanawake wana uwezekano mkubwa zaidi kuliko wanaume kuwekeza tena muda na pesa zozote walizonazo katika familia zao, na hasa afya na elimu ya watoto wao. Sekta za afya, elimu, na huduma za kijamii zingeanguka bila ushiriki wa wanawake.

Katika mipangilio ya ofisi, ni wanawake ambao mara kwa mara huchukua kazi zisizoonekana lakini muhimu ambazo huweka gia - kutoka kwa wafanyikazi wa ushauri hadi kazi ya usimamizi. Na timu zilizo na tofauti kubwa za kijinsia hufikia suluhisho za haraka na za ubunifu zaidi.

Upeo na athari za mgomo wa "Siku Bila Mwanamke" bado haujajulikana. Lakini tayari ni wazi kuwa wanawake wana nguvu kubwa ya kiuchumi.

Wanawake, kwa kweli, si waathirika walio katika mazingira magumu, lakini ni watunga-mabadiliko waliojitolea, wenye uwezo wa kuimarisha uchumi na kuendeleza maendeleo.

Hatuwezi kumudu kuendelea kudharau uwezo wa kiuchumi wa wanawake. Kama tunavyopenda kusema, wanawake huzaa, na zaidi ya watoto wachanga. Ni muhimu kwamba sisi, kwa upande wake, tuwafikishie.



# 4R za Samia darasa kwa demokrasia Tanzania

NA MWANDISHI WETU

DUNIA inashuhudia kufunguliwa kwa siasa za vyama vingi na shughuli zake katika ardhi ya Tanzania, si kwa kauli bali vitendo hasa baada ya wiki nzima kuwa na mvutano juu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutangaza maandamano ya amani.

Jina la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan litaendelea kutajwa kwenye midomo ya wapenda haki, wanaojua maana ya uhuru wa kujieleza na kutumia mbinu za maridhiano kuleta maendeleo ya nchi.

Wakati wa vuguvugu la kuanza upya mfumo wa vyama vingi nchini mnamo mwaka 1992, mambo kama haya yalikuwepo, mivutano, maandamano, askari kuwazuia wafuasi wa vyama vya siasa kwa mabomu ya machozi, risasi bandia au virungu.

Katika uchaguzi wa kwanza wa vyama vya siasa mwaka 1995, kiongozi wa upinzani Augustino Lyatonga Mrema aliyegombea urais kwa tiketi ya Chama cha NCCR-Mageuzi ndio alikuwa na wafuasi wengi. Kauli zake zilisikika na kufuatwa na kundi kubwa la wananchi kwa wakati huo.

Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), walijawa hofu; wakaona dhahiri mgombea wao Benjamin William Mkapa hatafua dafu. Wakaenda kwa Rais Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere kushitaki.

Majibu ya Mwalimu Nyerere yaliwanyongíonyeza wote waliomfuata, ambao walilalamika Mrema



anabebwa mabegani, akifika kwenye mkoa anatandikiwa khanga na gari kuzimwa huku akisukumwa.

Waliona hiyo ni ishara ya kuwavutia hata ambao walikuwa hawajui siasa ni nini wala nguvu au uwezo wa Mrema ni upi. Walitaraji majibu yatakayowapa faraja. Lakini Mwalimu aliwaambia kuwa Mrema aachwe abebwe, akasisitiza kuwa na yeyote anayetaka kubebwa kama maiti basi asizuiwe.

Masuala ya upinzani katika eneo lolote la nchi hayazuiliki, wakati Mwalimu Nyerere na wenzake wanapambana kupata uhuru wa Tanganyika kutoka kwenye makucha ya Waingereza katika miaka ya 1950; bado kulikuwepo na Waafrika waliozaliwa na kukulia Tanganyika waliunda vyama vya upinzani.

Baadhi ya vyama hivyo ni pamoja na African National Congress (ANC) cha Zuberi Mtemvu, All Muslim National Union of Tanganyika (AMNUT) ambacho kilikuwa chama cha Waislamu wazalendo wa Tanganyika pamoja na Tanganyika Democratic Party (TDP) cha Balozi Kasanga Tumbo huku vyama hivyo vikipewa nguvu na chama cha United Tanganyika Party (UTP) kilichoanzishwa na Gavana wa Tanganyika wakati huo Edward Twinning mwaka 1956 huku baadhi ya Waafrika wakiwa wanachama.

Utaona ni namna gani kina Mwalimu Nyerere walipata tabu kupambana na nguvu iliyotokana ndani yao (Waafrika),lakini baada ya kupata uhuru Disemba 9, 1961na kufanyika uchaguzi wa vyama vingi baadaye, ilipofika mwaka 1965 Mwalimu Nyerere akiwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliamua kufuta mfumo wa vyama vingi nchini ili kuleta utulivu wa kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Baadaye kutokana na takwa la kimataifa Tanzania iliamua kurejea kwenye mfumo wa vyama vingi mnamo mwaka 1992.

Hakuna kipindi kigumu katika uongozi wa Tanzania kama kuanzia mwaka 1992 hadi 2005. Mtikisiko mkubwa wa kisiasa ulipatikana, viongozi wa juu wakiongozwa na Mzee Ali Hassan Mwinyi (Rais wa Awamu ya Pili), Benjamin Mkapa (Rais wa Awamu ya Tatu) na baadaye Jakaya Kikwete (Rais wa Awamu ya Nne) walitumia uvumilivu wa hali ya juu kuhakikisha nchi inavuka salama; na walifanikiwa.

Hata hivyo, Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Pombe Magufuli alikuja na falsafa yake ñ alitaka utulivu wa kisiasa ili afanye maendeleo. Alichoshwa na kelele za wapinzani kudai mambo ambayo pengine aliona hayana msingi. Akazuia shughuli za kisiasa kuanzia maandamano, mikutano ya hadhara isipokuwa kwa wabunge wa jimbo husika pekee.

Kwa kipindi chote cha uongozi wake madarakani kuanzia Novemba, 2015 hadi mauti yalipomkuta Machi 18, 2021. Tanzania haikuwa na vuguvugu la kisiasa. Ingawa minongíono ilikuwa mingi.

Dk. Samia Suluhu Hassan alichukua kijiti na kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania manmo Machi 19, 2021. Matumaini mapya yakaanza kuonekana kwenye sura za Watanzania hasa viongozi wa vyama vya kisiasa.

Kila aliposimama kuzungumza na wananchi matarajio ni lini vyama vya siasa vitatoka kifungoni. Ndipo Januari 3, 2023 akatangaza kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa nchini na kuondoa marufuku iliyokuwepo kwa muda mrefu.

Rais Dk. Samia kauli hiyo aliitoa mbele ya viongozi wa kitaifa wa vyama vya siasa alipowaita Ikulu ya Dar es Salaam, alisema: ìUwepo wangu mbele yenu leo ni kuja kutangaza kwamba lile tangazo la kuzuia mikutano ya hadhara sasa linaondoka.îHiyo ilikuwa habari njema mbele ya viongozi wa vyama vikuu vya siasa za upinzani nchini.



# Ifahamu nguvu ya kisayansi 'inayoikinga' Pwani ya Afrika Mashariki na Vimbunga

NA MWANDISHI WETU

KWA mujibu wa vyanzo mbalimbali vya masuala ya hali ya hewa, kimbunga cha mwisho kuipiga Tanzania ilikuwa Aprili 14 mwaka 1952 mkoani Lindi, kipindi hicho bado ikiwa ni koloni la Tanganyika chini ya utaw ala wa Mwingereza.

Miaka 80 nyuma, yaani Aprili 15, 1872 kimbunga cha mwisho kiliipiga Zanzibar, na kwa mujibu wa maelezo yaliyorekodiwa ya Balozi wa Uingereza visiwani Zanzibar wa miaka hiyo Bw. John Kirk theluthi mbili ya mashamba ya minazi na karafuu visiwani humo yaliharibiwa vibaya.

Hivyo, laiti Jobo kingetua na nguvu, basi kingekuwa kimbunga cha kwanza kurekodiwa kupiga jiji la Dar es Salaam na cha pili kuipiga Zanzibar baada ya takriban miaka 149.

## Msimu wa vimbunga

Eneo la Bahari ya Hindi, kuanzia Kusini Magharibi ya India mpaka upwa wa Mashariki na Kusini ya Afrika una msimu wake wa vimbunga ambao huanza mwezi wa Novemba na kuishia mwezi wa Aprili.Vimbunga vya Zanzibar na Lindi vyote vilitokea mwezi wa nne, hata kwa upande wa Jobo pia huu ni mwezi wa Aprili.

Kimbunga Kenneth kilipiga mwezi wa Aprili 2019 na mwezi mmoja nyuma yake kimbunga kibaya zaidi cha Idai kiliipiga Msumbiji na athari zake kufika mpaka nchi jirani za Malawi na Zimbabwe. Zaidi ya watu 1,000 walipoteza maisha katika kipindi hicho.

Kwa msimu wa mwaka huu (2020/21) ambao unaelekea mwisho zaidi ya vimbunga vikubwa na hafifu 16 vimejitengeneza na kuathiri baadhi ya nchi katika ukanda huo, Jobo ikiwa ni kimoja wapo.

## Katikati ya dunia

Suala linalosalia ni kwa nini vimbunga hivyo havianzii ama kuathiri pwani ya Afrika Mashariki? Jibu ni kuwa eneo hilo lipo 'kati kati ya dunia'.

Dunia imegawanyika katika mihimili miwili, mhimili wa kusini na mhimili wa kaskazini. Kilichogawanyisha dunia katika mihimili hiyo ni mstari dhahania wa Ikweta. Mstari huo unapita kwenye nchi 13 duniani zikiwemo Somalia, Kenya na Uganda.

"Vimbunga husukumwa na nguvu iitwayo Kani ya Coriolis. Kani hiyo haina nguvu kabisa katika eneo la Ikweta kwa kuwa ndipo mhimili wa Kaskazini na Kusini huapaka, na upepo katika mihimili hiyo huenda katika njia tofauti upande mmoja kushoto upande mwengine kulia," anaeleza Profesa Marshall Shepherd, rais wa zamani wa Jumuiya ya Utabiri wa Hali ya Hewa ya Marekani.

Mtaalamu huyo anaeleza katika makala ya mwaka 2018 iliyochapishwa na jarida la Forbes kuwa nguvu hiyo kinzani ndio huua nguvu ya vimbunga katika eneo hilo.Japo Tanzania haijapitiwa na mstari wa Ikweta lakini ipo katika ukanda wa Ikweta, masafa machache kusini mwa mstari huo uliopita katika nchi jirani za Kenya, Uganda na hata DR Congo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Prof Shepherd endapo kimbunga kikali kitajitengeneza mbali na eneo hilo kinaweza kuathiri moja kwa moja eneo hilo, "japo kutokea kwa hali hiyo ingali bado ni jambo la nadra."Hata hivyo, hali ya mvua kubwa na mafuriko huukumba ukanda wa Ikweta kutokana na athari ya vimbunga vinavyopiga maeneo ya karibu katika msimu wake.



# Walijimilikisha nchi, Waarabu wenzao wakawaangusha

**KWA sasa Bashar al-Assad ameingia kwenye orodha ya viongozi mashuhuri wa nchi za Kiarabu waliopinduliwa tangu kuanza kwa maandamano katika nchi za kiarabu yapata mwongo mmoja nyuma**

.

Hadi mwisho wa 2010, wengi wa viongozi hawa wa nchi za Kiarabu, hawakuwahi kufikiria kwamba wangekumbana na mzozo ambao ungeangusha serikali zao.Nchi za Kiarabu za Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Afrika zilitikiswa na dhoruba ya mabadiliko ambayo yaling'oa viongozi ambao hapo awali walidhaniwa kuwa hawawezi kushindwa.

Mwenendo huu umeendelea hadi kiongozi wa mwisho ambaye aliondolewa madarakani na dhoruba ya mabadiliko, Rais wa Syria, Bashar al-Assad.

Zine al-Abidine Ben Ali (Tunisia, 2011)

Rais wa zamani wa Tunisia, Zine al-Abidine Ben Ali, alikuwa kiongozi wa kwanza wa nchi ya Kiarabu ambaye Serikali yake ilipinduliwa baada ya dhoruba ya mapinduzi wa kiraia.

Zine al-Abidine Ben Ali, aliitawala Tunisia kwa miaka 23, alikimbia na familia yake hadi Saudi Arabia Januari 2011 baada ya maandamano ya mwezi mzima dhidi ya serikali yake, ambayo yalichochea wimbi la mapinduzi katika nchi za Kiarabu.Waandamanaji hao waliishutumu serikali yake kwa kushindwa kutoa ajira kwa raia wengi wa nchi hiyo hasa vijana na kuwashutumu maafisa wa serikali kwa ufisadi.

Maandamano hayo yalizuka baada ya kijana mmoja kujichoma moto baada ya kudhulumiwa na polisi Desemba 17, 2010.Mohamed Bouazizi alifariki Januari 4, 2011, lakini kujitoa kwake kulisambaa kwenye mitandao ya kijamii, na hivyo kuzua ghasia za umma zilizompindua Zine El Abidine Ben Ali.

**Hosni Mubarak (Misri, 2011)**

Hosni Mubarak alitawala Misri kwa miaka 30 kabla ya maasi ya nchi za Kiarabu. Mabadiliko ya serikali nchini Tunisia yalichochea kuondolewa Mubarak nchini MisriMubarak alijiuzulu baada ya wiki kadhaa za maandamano dhidi ya serikali yake, yaliyoanza Januari 25 katika uwanja wa Tahrir mjini Al Khahira.

Waandamanaji hao waliishutumu serikali yake kwa kushindwa kutatua tatizo la ukosefu wa ajira, ongezeko la umaskini na kukithiri kwa rushwa.

**Ali Abdullah Saleh (Yemen, 2011)**

Baada ya miezi kadhaa ya maandamano yaliyopindua serikali za nchi za Kiarabu, dhoruba hiyo ilifika Yemen, ambapo baada ya miezi kadhaa ya upinzani kati ya wananchi na serikali, Rais Ali Abdullah Sale alikubali kung'atuka madarakani.

Ali Abdullah Sale alikubali kukabidhi madaraka kwa makamu wake, Abd-Rabbu Mansour Hadi, baada ya maandamano ya ghasia yaliyopelekea shambulio la bomu kwenye ikulu ya rais.

Aliondoka madarakani Novemba 23, 2011, baada ya kupona majeraha aliyoyapata wakati wa shambulio la bomu kwenye ikulu yake, na shinikizo kutoka ndani na nje ya nchi.

**Muammar Gaddafi (Libya, 2011)**

Wimbi hilo la mabadiliko lilifikia Libya ambapo liliipindua serikali ya kiongozi wake aliyekaa madarakani kwa muda mrefu zaidi, Muammar Gaddafi, baada ya kuwa madarakani katika nchi hiyo kwa miaka 42.

Muammar Gaddafi alikuwa kiongozi wa kwanza kuuawa baada ya wimbi la kupinduliwa kwa tawala katika nchi za Kiarabu.Muammar Gaddafi aliingia madarakani Septemba 1969 baada ya mapinduzi ya ghafla, na kumuangusha mfalme Idris anayeungwa mkono na Uingereza.

Wakati akiwa madarakani, Gaddafi alishutumiwa kuwaunga mkono waasi katika nchi nyingine, na moja ya mambo aliyojizolea umaarufu nayo ni kuhusika kwake katika kulipua ndege ya Pan Am katika anga ya Lockerbie, Scotland, Disemba 1988.

Shambulio hilo liliua abiria wote 259 waliokuwa ndani ya ndege hiyo, 190 kati yao walikuwa Wamarekani.

Maandamano dhidi ya serikali yake yaligeuka kuwa vita vya wenyewe kwa wenyewe, ambapo vikosi vya serikali na waasi vilipigana kwa muda wa miezi minane.

Oktoba 20, 2011, wapiganaji waasi walitangaza kifo cha Gaddafi, ambaye walisema aliuawa katika mji alikozaliwa, Sirte. Aliuawa akiwa na umri wa miaka 69.

Hata hivyo, wapo wanaomwona kuwa ni mtu aliyejaribu kuunganisha bara la Afrika. Katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 2009, Gaddafi alitoa hotuba kwa zaidi ya saa moja, jambo ambalo lilikuwa kinyume na kanuni.

Aliikosoa mfumo wa kura ya turufu ya viti vya nchi tano katika baraza ya Umoja wa Mataifa na kutaka mfumo huo ufutwe. Kisha akakosoa vikali hatua ya Marekani kuvamia nchini Iraq.

**Bashar al-Assad (Syria, 2024)**

Rais wa hivi karibuni zaidi ambaye serikali yake ni Bashar al-Assad, baada ya kundi la waasi kuongoza maasi dhidi ya serikali yake Jumapili, Desemba 8, 2024. Familia ya Assad imeitawala Syria kwa miaka 53.Rais Bashar al-Assad alichukua madaraka mwaka 2000, baada ya babake kutawala kwa miaka 30.

Miaka 13 iliyopita, alitumia nguvu kuwakandamiza waandamanaji, na kisha kukawa na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Zaidi ya watu nusu milioni wameuawa, na wengine milioni 12 wamelazimika kukimbia makazi yao.Kundi la Kiislamu, Hayat Tahrir al-Sham (HTS) lilifanikiwa kufanya mashambulizi mabaya kaskazini magharibi mwa nchi hiyo, baada ya kushirikiana na makundi mengine ya waasi.

Waasi hao waliuteka mji wa pili kwa ukubwa nchini Syria, Aleppo na kuelekea kusini hadi mji mkuu, Damascus, ambako walizidi nguvu jeshi la Syria.Urusi baadaye ilitangaza kuwa Assad na familia yake wamepewa hifadhi ya kisiasa huko Moscow.



# Siku niliyoduwazwa na mlemavu wa macho shabiki wa Pacome

**MAFANIKIO ya mpira huwa ni process vinginevyo labda iwe fluku.Kwenye mpira fluku ipo. Ligi ya Uingereza Leicester ilikutana na fluku ikatwaa ubingwa na baada ya hapo misimu miwili mbele ilishuka daraja.Unaweza kupata fluku msimu mmoja ukafika fainali ya shirikisho ila Kwa kuwa ni fluku misimu miwili mbele ukashindwa kuvuka makundi.**



Kuna presha inatengenezewa mashabiki wa Simba kwamba Sasa ionekane kucheza robo fainali ni hatua ndogo na haina faida yoyote bali mnatakiwa kufika fainali sababu tu kuna waliofika Kwa fluku.

Mkiikubali hiyo presha na mkasahau zaidi 70% ya wachezaji wenu ndio kwanza msimu wakwanza wanacheza Simba na mkasahau hata benchi la ufundi ni jipya na ndio kwanza linaitafuta Simba tunayoitaka. Ni kwamba ghafla mtahama kuwa wavumilivu na timu yenu na mkaanza kudai mafanikio ambayo yatakuwa ni sawa na kutaka kuhamia nyumba mpya ambayo haijakamilika kujengwa.

Ukiniuliza Mimi nitakwambia timu ipo kwenye njia sahii ya kujengwa upya na hapa tulipo tunakula bonus ambayo Wala hatukuitarajia.

Tunachopaswa kufanya Kwa Sasa ni kuiunga mkono timu yetu Kwa nguvu zote na kuipambania iendelee kufanya vizuri bila kuwapa presha yoyote viongozi, benchi la ufundi Wala wachezaji.

Tukikubali kujazwa upepo wa presha na tukaanza kupeleka presha Kwa benchi la ufundi na wachezaji tukawaondolea utulivu wakaanza kucheza Kwa presha ya matokeo na kulazimisha mambo tutaharibu.

Kwa Sasa lazima tukubali Simba imetuheshimisha na tuendelee kuwapa morali wachezaji wetu waendelee kupambana wakijua tupo nyuma Yao katika mazingira yoyote bila kuwapa presha hata chembe.

Tuwaache wanaopenda fluku waendelee kusubiri fluku nyingine huku sisi tukikubali mpira ni process na tunajua taratibu tutafika tunapokwenda. Tulitengeneza timu iliyotupa mafanikio ikafika mahali ikafika mwisho ikachoka na tukaibomoa. Imetuchukua misimu mitatu kuanza kuona timu mpya yenye matumaini inajengwa upya.

Tuweni na subira na tusikubali kabisa kutiwa ndimu na wanaotaka kututia presha tuanze kuhamaki na kuhama kwenye lengo.

(***Jicho la tatu la Mgalilaya).***

kumekucha @kumekucha @kumekucha
mwanzo mpya
# KUMEKUCHA



# SIMBA SC YAANZA HESABU ZA UBINGWA

NA MWANDISHI WETU

WAKATI Ligi Kuu ya Tanzania ndiyo kwanza inaingia katika mzunguko wa pili, Klabu ya Simba imejigamba kuwa itaendeleza ubabe na kutwaa ubingwa msimu huu iwe isiwe.
Simba inaongoza ligi hiyo imesisitza kuwa msimu huu imejipanga kila idara ikiwemo kuwana wachezaji wenye viwango, benchi bora la ufundi pamoja na uongozi shupavu chini ya Mwekezaji Mohamed Dewji Mo.

Meneja wa habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo Ahmed Ali aliwaambia wanachama na wapenzi wa Simba mjini Zanzibar kuwa machungu waliyokuwa nayo ya kupoteza ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo, sasa yamefikia tamati na kinachokuja mbele yao ni furaha.

Simba inaendelea na kampeni ya kufungua matawi na kuhamasisha wanachama kulipia kadi zao ili kuendelea kuimarisha klabu hiyo kongwe Tanzania.

Simba ndiyo timu pekee katika Tanzania iliyobakia katika ushiriki wa michuano ya kimataifa, baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya Robo Fainali ya Michuano ya Kombe la Shirikisho.

# FADLU ACHIMBA MKWARA

NA MWANDISHI WETU

KOCHA Mkuu wa Simba Fadlu Davis amewapiga mkwara wachezaji wake akidai kwamba ataanza falsafa ya kuwachezesha nyota wake watakaompa matokeo mazuri katika mazoezi na siyo vingine
Kocha huyo amesema katika kazi yake hiyo huwa hana historia ya kuangalia wasifu wa mchezaji na badala yake anaangalia kazi anayoifanya katika uwanja wa mnazoezi na kuchukua kama ndiyo kigezo cha kufanya naye kazi.
Kocha huyo Raia wa Afrika Kusini amesema anafanya hivyo kutokana na ukweli kwamba kikosi chake hakina mapungufu ya mchezaji wa eneo fulani, bali kinachotakiwa ni kuwafanya wacheze kitimu, hivyo ana kazi kubwa ya kutafuta muunganisho wa kikosi chake.
Hiyo imetokana na kile alichodai kwamba usajili wao ulizingatia kila eneo, huku Kamati iliyofanya kazi hiyo ikijaribu kupata wachezaji wazuri kutoka timu mbalimbali, ambao walihitaji kuwaunganisha, zoezi ambalo linakwenda vizuri.
Katika mkakati huo Fadlu amewahakikishia mashabiki wa Simba kuwa kiungo wao hatari Elie Mpanzu katika mechi zijazo wataanza kumuona akianza kikosi cha kwanza kutokana na kuzoea na kupata pumzi ya kutosha tofauti na ilivyokuwa hapo awali.
Mpanzu alikuwa akitumiwa sana kucheza dakika chache za mwanzoni au mwisho, ambapo sasa ataonekana akiongezewa muda wa kuitumikia timu yake hiyo aliyoijiunga nayo akitokea AS Cita ya nchini DRC.

# TETESI ZA USAJILI

## Nkunku anasa rada za Man UTD

Manchester United huenda ikamsajili mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa Christopher Nkunku, 27, kwa mkopo ikiwa Muingereza Marcus Rashford, 27, ataondoka katika klabu hiyo. (The Athletic – Usajili unahitajika)





## Bayer Munich yamtolea macho James Mcattee

Bayer Leverkusen wamefanya mawasiliano na Manchester City kuhusu uhamisho wa mkopo wa kiungo wa kati wa England chini ya umri wa miaka 21 James McAtee, 22. (Daily Mail).